BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com


**HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.**

**Mheshimiwa Spika,**

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema na utukufu kwa kutuwezesha kukutana tena leo hii, katika chombo hiki muhimu tukiwa wazima wa afya kwa lengo la kutekeleza majukumu yetu ya kikatiba ya kuwatumikia wananchi katika Mkutano huu wa Bajeti unaotuelekeza kujadili, kushauri na hatimae kupitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inachukua fursa hii kuwapongeza viongozi wetu wakuu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa mafanikio makubwa yaliyoyapatikana katika kuutangaza utalii nchini kupitia Filamu ya Royal Tour. Idadi ya watalii wanaoingia nchini inaonekana kuongezeka siku hadi siku, hali inayochangia kukua kwa pato la taifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu pia inatoa pongezi kwa Makamo wa kwanza wa raisi Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah, kwa namna wanavyoshirikiana vyema na Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu mazito ya Kitaifa katika kuijenga nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**,

Aidha, naomba kumshukuru pia Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mheshimiwa Simai Mohamed Said, Katibu Mkuu Bibi Fatma Mabrouk Khamis, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Amina Ameir Issa, Afisa Mdhamin ndugu Zuhura Mgeni Othman, Wakurugenzi pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa mashirikiano makubwa waliyotupatia wakati wa kuchambua na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**,

Kwa niaba ya Kamati ya Kilimo Biashara na Utalii, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi **Mheshimiwa Spika**, Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika, Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Wenyeviti wa baraza, Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma pamoja na Mheshimiwa Abdalla Hussein Kombo kwa juhudi na maarifa yenu makubwa mnayoendelea kuyatumia wakati mkiliongoza Baraza hili.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, ambao wamejitoa kwa hali zote katika kuisaidia Serikali kutimiza malengo yake. Michango yao pamoja na uchambuzi wa kina walioutoa kuhusiana na bajeti hii, utasaidia sana katika kutekeleza malengo mazuri ambayo Wizara hii imejipangia kwa mwaka wa fedha ujao.

**Mheshimiwa Spika**,

Kwa heshima kubwa kabisa naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Yussuf Hassan Idd | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Azza Januari Joseph | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Mwanajuma Kassim Makame | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Said Saleh Salim | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Abuubakar Mahmoud Idd | Katibu |
| 8. | Ndg. Mwaka Mwinyi Waziri | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya shukurani hizo, naomba sasa niende moja kwa moja kwenye uwasilishaji wa Maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii iliipitisha bajeti ya Wizara hii kwa kutoa maelekezo na ushauri kidogo, ambao Wizara iliahidi kuufanyia kazi ili malengo ya mwaka huu wa kibajeti yaweze kukamilika kwa wakati. Kwa mwaka 2023/2024 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imepanga kutekeleza malengo yake kupitia Programu kuu tano kama zifuatazo:

i) Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe;

ii) Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii;

iii) Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii;

iv) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Utalii, na

v) Programu ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE

**Mheshimiwa Spika,**

Lengo kuu la Programu hii ni kuwa na Mji Mkongwe na maeneo ya kihistoria yaliyohifadhiwa, kuimarishwa na kuendelezwa kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadae. Matokeo ya muda mrefu ni kuyahifadhi, kuyalinda, na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini pamoja na uhifadhi wa Mji Mkongwe ili uweze kubakia kuwa ni urtithi wa kitaifa, kikanda na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatoa pongezi zake za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya uongozi wake Mheshimiwa Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa maamuzi yake sahihi ya kulikarabati jengo la Bait el Ajaib liliopo Forodhani Unguja, kwa lengo lilelile la kuyahifadhi, kuyalinda, na

kuyaendeleza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini, pamoja na uhifadhi wa Mji Mkongwe ili uweze kubakia kuwa ni urtithi wa kitaifa, kikanda na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Moja kati ya vipaumbele vya msingi ambavyo wizara ya Utalii imejipangia kuvitekeleza kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni ukarabati wa ujenzi wa jengo la Bait el Ajaib, ikiwa ni katika hatua za kuyalinda na kuyahifadhi maeneo ya mji Mkongwe. Katika kulitekeleza hili, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, kumsimamia kwa karibu sana Mkandarasi wa ujenzi wa jengo hili, ili ukarabati wa jengo hili uweze kukamililka kwa wakati uliopangwa na thamani ya fedha halisi itakayotumika iweze kuonekana.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, katika kuhakikisha kuwa ukarabati huu unafanikiwa, umakini mkubwa unahitajika hasa tukizingatia hali halisi ya jengo lilipo. Kwa mujibu wa maelezo ya wataalamu ni kwamba, maji yanapatikana karibu mita nne (4m) kwenda chini ya jengo hili, hivyo ni vyema Mkandarasi akasimamiwa katika matumizi sahihi ya vifaa katika ujenzi wa jengo hili, ili kuepusha hasara na maafa zaidi kam yale yaliyotokezea hapa awali.

**Mheshimiwa Spika,**

Ukarabati wa ujenzi wa jengo la Bait el Ajaib liliopo Forodhani Unguja, umesainiwa tarehe 13/02/2023 baina ya Serikali ya Ufalme wa Omani na Kampuni ya Nandhra Engineering and Construction Company Limited ya Tanzania, ambapo Mheshimiwa Simai Mohamed Said alishiriki katika kusaini makubaliano hayo kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ukarabati huu utagharimu jumla ya dola za Kimarekani Milioni 21. Ujenzi ambao unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu na kwa hivi sasa Mkandarasi ameshakabidhiwa jengo na yupo katika hatua za matayarisho.

## PROGRAMU YA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII

**Mheshimiwa Spika,**

Matokeo ya muda mrefu katika utekelezaji wa Programu hii ni kuwa na utalii endelevu na wenye tija kwa maslahi ya nchi na wananchi wake. Katika kuyafikia malengo haya, Idara ya Utalii inalazimika kuibua vivutio vingi zaidi vya utalii nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza kwa dhati Wizara ya Utalii kupitia Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba kwa juhudi inazoendelea kuzichukuwa katika kulitekeleza jukumu hili. Kamati imefarijika na imeriridhika juu ya hatua nzuri ya ongezeko la vivutio vipya vya Utalii kisiwani Pemba, ambavyo kwa njia moja au nyengine vitaweza kukinyanyua kisiwa cha Pemba kiutalii, hali itakayochangia kwa kiasi kikubwa katika kuongeza pato ya Taifa na upatikanaji wa ajira

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na umuhimu wa vivutio hivi, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kushirikiana na jamii kisiwani Pemba katika kuibua vivutio zaidi na ijipange katika kuendelea kutoa uelewa kwa jamii kupitia jumuiya mbalimbali ziliomo nchini, masheha pamoja na viongozi wa majimbo Aidha, Wizara ijipange katika kuviimarisha vivutio hivyo ili malengo ya uvumbuzi huo yaweze kufikiwa hasa tukizingatia kwamba, jamii zinaonekana wazi kwamba ziko tayari kushirikiana na Serikali yao katika kulifanikisha suala hili. Kuimarika kwa vivutio hivi kutaiwezesha Serikali kupitia Wizara ya Utalii kuongeza idadi ya vyanzo vyake vya mapato, ambapo wageni wengi kutoka ndani na nje ya nchi watakapoweza kufika katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuhakikisha kwamba, idadi ya wageni wanaoingia nchini inaongezeka, suala la usafi linapaswa kupewa kipaumbele zaidi katika maeneo yote ya utalii. Katika kulifanikisha hili, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kupitia Idara ya Utalii, kuendelea kushirikiana kwa dhati na wadau wa utalii pamoja na taasisi binafsi, kuhakikisha kwamba usafi unaimarika katika maeneo yote ya Utalii kwa lengo la kuwavuta zaidi wageni waweze kufika katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kulifanikisha hilo, Kamati inaishauri Serikali kwa kusihirikiana na Wizara ya Miundombinu kuharakisha mchakato wa upanuzi wa kiwanja cha ndege - Pemba ili kutoa fursa kwa ndege kubwa za kimataifa kuweza kutua katika uwanja huo, hali itakayoruhusu wageni kutoka nje ya nchi kufika moja kwa moja kisiwani humo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kikosi cha Utalii na Diplomasia kilichoanzishwa kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama wa wageni nchini, kinaonekana kuwa na tija kubwa katika kuiendeleza na kuiimarisha sekta ya Utalii nchini, kwa kufanikiwa kufanya doria katika maeneo mbalimbali ya Utalii kisiwani Unguja ikiwa ni pamoja na maeneo ya Mji Mkongwe, Uwanja wa Ndege, Jambiani, Paje, Uroa na Michamvi.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na hali hiyo ipo haja ya kikosi hicho kuanzishwa kisiwani Pemba kama Wizara ilivyojipangia kulitekeleza hili kwa mwaka wa fedha unaokuja, hasa tukizingatia kwamba, Serikali imelenga kukifungua Kisiwa cha Pemba kiutalii. Hivyo ni vyema kabisa wageni watakaofika kisiwani humo wakahakikishiwa ulinzi na usalama wao pamoja na mali zao.

**Mheshimiwa Spika,**

Hivyo,Utekelezaji wa suala hili muhimu kwa maendeleo ya Utalii, yatafanikiwa endapo Serikali kupitia Wizara ya Fedha itaingiza fedha zilizopangwa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii utekelezaji wake unahitaji fedha nyingi ingawa bajeti iliyopangwa kwa mwaka huu wa fedha ni finyu ukilinganisha na uzito wa malengo yaliyowekwa. Jumla ya shilingi za Kitanzania **Milioni 658, 677,000** zimepangwa kutumika kwa mwaka huu 2023/2024. Kwa mnasaba huo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuwaingizia fedha hizo kwa wakati ili waweze kutekeleza malengo waliyojipangia.

## PROGRAMU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI UTALII

**Mheshmiwa Spika,**

Utekelezaji wa Programu hii unalenga kuongeza uelewa kwa wakaazi wa Tanzania pamoja na jamii ya kimataifa, kuhusu bidhaa na huduma za Utalii ziliopo Zanzibar. Kamisheni ya Utalii ndio kiungo kikuu cha utekelezaji wa malengo hayo, ambapo kwa muda mrefu inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti unaokwamisha utekelezaji wake.

**Mheshmiwa Spika,**

Kamati inaipongeza kwa dhati Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya uongozi wake Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuiridhia Kamisheni kukusanya mapato kupitia vyanzo vyake na kutumia mapato hayo katika kuitangaza Sekta ya Utalii katika anga za kitaifa na kimataifa.

**Mheshmiwa Spika,**

Kwa mnasaba huo, Kamati inaishauri Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuwa wabunifu na kuongeza juhudi zaidi katika kutekeleza majukumu waliojipangia kwa lengo la kupiga hatua kubwa zaidi katika ukusanyaji wa mapato yake.

PROGRAMU YA UTAWALA NA UENDESHAJI NA URATIBU WA UTALII

**Mheshmiwa Spika,**

Programu hii imelenga kuongeza tija katika sekta ya Utalii nchini pamoja na kuweka mazingira bora ya rasilimali watu katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya utalii.

**Mheshmiwa Spika,**

Katika kuhakikisha kwamba watumishi wanafanikiwa katika utekelezaji wa majukumu yao, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale haina budi kuhakikisha kwamba, inaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wake kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kiutendahi. Aidha kutoa fursa kwa watumishi hao kuweza kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanayoendelea kukuwa siku hadi siku.

**Mheshmiwa Spika,**

Utekelezaji wa mipango ya Wizara iliyojipangia kupitia Programu hii inahitaji fedha za kutosha, ambapo kwa mwaka huu wa fedha 2023/2024, Programu imepangiwa jumla ya shilingi za kitanzania **bilioni 3,238,154,000** fedha ambayo imeongezeka kidogo ukilinganisha na fedha iliyotengwa kwa mwaka uliopita, 2022/2023 ambayo ilikuwa ni jumla ya shilingi za kitanzania **bilioni 2,775,713,000.**

HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale katika Baraza lako tukufu, pia niwashukuru Wajumbe wako wote kwa utulivu wao waliouonesha wakati nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Nawaomba Wajumbe wako waichangie bajeti hii, wahoji, waijadili na watoe mapendekezo yao pale panapohitajika na hatimaye kuipitisha baada ya kuafikiana kwa hoja mbali mbali watakazoziibua wakati wa mjadala.

**Mheshimiwa Spika**,

naomba kuwasilisha.

……………………………………….

**Yussuf Hassan Idd,**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar.**